



JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO



Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W)

Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo

S. L. P. 02,

TUKUYU

04.08.2023

**TANGAZO LA AJIRA ZA MKATABA UJEZI NA
UKARABATI WA MIUNDOMBINU YA SHULE YA
SEKONDARI MWAKALELI**

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo anapenda kuwatangazia wananchi wote kuwa anatarajia kufanya shughuli za ujenzi wa mabweni mapya manne(4) na ukarabati wa miundombinu mbalimbali katika Shule ya Sekondari Mwakaleli kama ilivyoainishwa hapo chini. Hivyo basi Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo inakaribisha maombi ya ajira ya Mkataba wa muda mfupi kwa ajili ya utekelezaji wa kazi hizo kwa mafundi wenye uzoefu katika fani zifuatazo

- i. Fundi uwashi
- ii. Fundi umeme
- iii. Fundi Aluminium (awe na EFD Machine)
- iv. Fundi seremala

Kwa ajili ya kufanya kazi zifuatazo:-

- i. Ukarabati wa bweni la wavulana (Paradiso)
- ii. Ukarabati wa bweni la wasichana (Mpombo)
- iii. Ujenzi wa bweni jipya la Wasichana (1)

- iv. Ujenzi wa mabweni mapya ya Wavulana (2)
- v. Ujenzi wa bweni jipya la wanafunzi wenye mahitaji maalum Wavulana (1)
- vi. Ukarabati wa block ya vyumba viwili vya madarasa na ofisi (form three & four classrooms)
- vii. Ukarabati wa block ya vyumba viwili vya madarasa na ofisi (form one classrooms)
- viii. Ukarabati wa block ya vyumba vitatu vya madarasa.
- ix. Ukarabati wa block ya vyumba vinne vya madarasa na ofisi (form five & six classrooms)
- x. Ukarabati wa chumba kimoja cha maabara ya biology
- xi. Kutengeneza na kufitisha madirisha ya Aluminium
- xii. Kusuka mfumo wa umeme
- xiii. Kutengeneza na kupachika fremu na top za milango

SIFA ZA MUOMBAJI


- i. Mwombaji lazima awe raia wa Tanzania mwenye umri wa kuanzia miaka 18 na kuendelea
- ii. Mwombaji lazima awe na namba ya utambulisho ya mlipa kodi (Tin Number)
- iii. Mwombaji lazima awe na akaunti ya benki iliyo hai
- iv. Mwombaji lazima andike barua ya maombi kwa jina lake na siyo Kampuni au jina la biashara
- v. Mwombaji awe na ujuzi wa kusoma ramani na kuilezea.
- vi. Mwombaji awe tayari kufanya kazi muda wote hadi hapo mradi utakapo kamilika bila visingizio.
- vii. Mwombaji awe amewahi kufanya kazi ya ujenzi wa majengo ya serikali na mwenye uelewa na taratibu zake, ambatanishe nyaraka muhimu ili kuthibitisha kuwa amewahi kufanya kazi za serikali, nakala kama Mkataba wa kazi, Hati za malipo katika kipindi cha kuanzia mwaka 2019 mpaka 2023
- viii. Mwombaji lazima ambatanishe barua ya utambulisho kutoka Ofisi ya Mtendaji Kijiji/Mtaa
- ix. Mwombaji awe na mtaji wa kuwalipa mafundi bila kulipwa malipo ya awali (Advance payment)
- x. Aidha mafundi watakaopata kazi watatakiwa kuajiri mafundi wengine na wasaidizi wao kutokana na uhitaji wa kazi husika.

MASHARTI YA MUOMBAJI

- i. Mwombaji atatakiwa kulipia Gharama ya maombi ya kazi kiasi cha shilingi za kitanzania eifu ishirini tu (20,000/=) kabla ya kuwasilisha barua ya maombi.
Malipo yote ya maombi ya kazi yalipwe kwenye Account ya Halmashauri, Kabla ya kuwasilisha barua ya maombi malipo waombaji watafika Ofisi ya mapato iliyopo Halmashauri ili wapate namba ya kumbukumbu (Control Number)
- ii. Maombi yote yawasilishwe Ofisi ya Mkurugenzi Mtendaji (W), Halmashauri ya Wilaya ya Busokelo P. O. Box 02, Tukuyu. Mwisho wa kupokea maombi haya ni tarehe 15/08/2023 saa 9.30 alasiri.

NB:

1. Maombi yote ambayo hayataambatanishwa na nyaraka zilizoorodheshwa katika sifa za mwombaji hayatafanywa kazi.
2. Usaili utafanyika katika shule ya sekondari Mwakaleli siku moja baada ya kufungwa kwa dirisha kupokea maombi siku ya Jumatano tarehe 16/08/2023, kuanzia saa 04.00 asubuhi.


Samwel Oberlin

KAIMU MKURUGENZI MTENDAJI (W),
HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSOKELO

**MKURUGENZI MTENDAJI (W)
BUSOKELO**